Ni Wakati Wa Kuamka!

na

Ellis P. Forsman

Ni Wakati Wa Kuamka!

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 12, 2011

Ni Wakati Wa Kuamka!

Rum. 13:11-14

Hali ya kutojali na uzito ndiyo matatizo yanayowasumbua watu wa Mungu. Wakristo wengi kwa urahisi "wanakwenda kupitia hisia".

Makanisa mengi yapo, lakini kwa shauku ndogo au maendeleo madogo. Matatizo kama haya yalikuwa sugu wakati wa Agano Jipya. Kanisa la Waefeso liliacha upendo wao wa kwanza. Ufu. 2:4, "*Lakini nina neno juu yako, ya kwamba umeuacha upendo wako wa kwanza.*"

Kanisa la Laodikia lilikuwa vuguvugu. Ufu. 3:15-16, "*Nayajua matendo ya kuwa hu baridi wala hu moto; ingekuwa heri kama ungekuwa baridi au moto. Basi, kwa sababu una uvuguvugu, wala hu baridi wala moto, nitakutapika utoke katika kinywa changu.*"

Paulo alikuwa na hitaji la kuwahimiza ndugu katika Rumi kuamka kutoka usingizini. Rum. 13:11-14, "*Naam, tukiujua wakati, kwamba saa ya kuamka katika usingizi imekwisha kuwadia kwa maana sasa wokovu wetu u karibu nasi kuliko tulipoanza kuamini usiku umeendelea sana, mchana umekaribia, basin a tuyavue matendo ya giza, na kuzivaa silaha za nuru. Kama ilivyohusika na mchana na tuenende kwa adabu; si kwa ulafi na ulevi, si kwa ufisadi na uasherati, si kwa ugomvi na wivu. Bali mvaeni Bwana Yesu Kristo, wala msiuangalie mwili, hata kuwasha tamaa zake.*"

Je tumekuwa wazito na tofauti katika vitu vya milele? Kama ndivyo, "Ni Wakati Wa Kuamka!" Pamoja na uhimizo wa Paulo, zingatia baadhi ya sababu.

Kwa nini tunahitaji kuamka

Rum. 13:11-12, "*Naam, tukijua wakati kwamba saa ya kuamka katika usingizi umekwisha kuwadia; kwa maana sasa wokovu wetu u karibu nasi kuliko tulipoanza kuamini. Usiku umeendelea sana mchana umekaribia, basi na tuyavue matendo ya giza, na kuzivaa silaha za nuru.*"

"*Tukijua wakati*".

Tukifahamu uasili wa nyakati. Wakati ni mfupi. Wakati unaendelea. Yako. 4:14-17, "*Walakini hamjui yatakayo kuwako kesho. Uzima wenu ni nini? Maana ninyi ni mvuke uonekanao kwa kitambo kisha hutoweka. Badala ya kusema, Bwana akipende, tutakuwa hai na kufanya hivi na hivi. Lakini sasa mwajisifu katika majivuno yenu; kujisifu kote kwa namna*

hii ni kubaya. Basi yeye ajuaye kutenda mema, wala hayatendi, kwake huyo ni dhambi."

Tukijua ni wakati gani. Sasa ndiyo wakati wa kumtii Bwana. Sasa ndiyo wakati wa kutii wokovu. 2 Kor. 6:1-2, "*Nasi tukitenda kazi pamoja naye twawasihi msiipokee neema ya Mungu bure. (Kwa maana asema wakati uliokubalika nalikusikia, siku ya wokovu nalikusaidia; tazama wakati uliokubalika ndio sasa; tazama, siku ya wokovu ndiyo sasa.)*"

"*Sasa wokovu wetu hu karibu*".

Wokovu wetu hu karibu – kwa njia gani? Wakati wa kurudi kwa Bwana u karibu. Kifo chetu wenyewe kiko karibu, tunapaswa kufa kabla ya kurudi kwa Bwana. Ebr. 9:27, "*Na kama vile watu wanavyowekewa kufa mara moja, na baada ya kufa hukumu.*"

Badala ya sisi kuamini kwanza.

Kila siku hutuleta karibu. Fikiria juu ya kiasi cha muda uliokwenda toka tulipoamini!

"*Usiku umeendelea sana*".

Usiku – ikimaanisha matendo ya giza ya ulimwengu huu. 1 Yoh. 2:8, "*Tena nawaandikia amri mpya, neno lililo kweli ndani yake na ndani yenu; kwa kuwa giza linapita na lile nuru ya kweli imekwisha kung'aa.*"

Umeendelea sana – kwa ualisia, "imekatwa". Inakuwa fupi; inakaribia kwisha. 1 Kor. 7: 31, "… *kwa maana mambo ya ulimwengu huu yanapita.*"

Ulimwengu huu na wakati kama tunavyojua havitachukua muda mrefu.

"*Mchana umekaribia.*"

Siku ya baraka za kiroho imekaribia – ipokaribu kupambazuka katika ufufuo wetu wa milele.

2 Pet. 1:19, "*Nasi tuna lile neno la unabii lililo imara zaidi, ambalo mkiliangali, kama taa ing'aayo mahali penye giza, mwafanya vyema mpaka kutakapopambazuka na nyota ya asubuhi kuzuka mioyoni mwenu.*"

Tunavyopaswa kutembea

Rum. 13:12-14, "*Usiku umeendelea sana, mchana umekaribia, basi na tuyavue matendo ya giza na kuzivaa silaha za nuru. Kama ilivyohusika na mchana na tuenende kwa adabu; si kwa ulafi na ulevi, si kwa ufisadi na uasherati, si kwa ugomvi na wivu. Bali mvaeni Bwana Yesu Kristo, wala msiuangalie mwili, hata kuwasha tama zake.*"

"*Tuyavue matendo ya giza*"

Mambo kama yalivyoonyeshwa katika kifungu hiki:

- Ugomvi (kelele, ulevi, na mabishano – Kamusi ya Strong).
- Ulevi.
- Kuruka ruka (matendo ya zinaa, uchafu).
- Hamu (tama ya ngono).
- Mvutano (kubishana, mapigano).
- Wivu (kutaka, kumtaka mtu au kitu ambacho mtu mwingine anayo).

Mambo kama hayo yameonyeshwa katika vifungu vingine:

Gal. 5:19-21, "*Basi matendo ya mwili ni dhahiri ndiyo haya, uasherati, uchafu, ufisadi, ibada ya sanamu, uchawi, uadui, ugomvi, wivu, hasira, fitina, faraka, uzushi, husuda, ulevi, ulafi, na mambo yanayofanana na hayo, katika hayo nawaambia mapema, kama nilivyokwisha kuwaambia ya kwamba watu watendao mambo ya jinsi hiyo hawataurithi ufalme wa Mungu.*"

- Uasherati (uhusiano wa kimapenzi na mke wa mtu).
- Uzinzi (uhusiano wa kimapenzi wa aina yo yote – ni neno pana).
- Uchafu (mchafu, mawazo yaliyojaa tama).
- Uliyokithiri (Haiwezi kuzuilika, tama iliyozidi).
- Ibada ya sanamu (kuabudu mungu bandia).
- Uchawi (matendo ya giza).
- Chuki.
- Utofauti (ugomvi, mvutano).
- Hasira.

- Sifa (kujiinua mwenyewe, ubinafsi).
- Maasi (kutofautiana).
- Kikundi (watu wengi wanaofuata matakwa yao wenyewe; zaidi sana kuvamia mji).
- Kuwa na wivu (kutaka, kutamani kitu alicho nacho mwenzako).
- Uuaji.
- Ulevi.
- Na mengine yanayofanana na hayo.

Kol. 3:5-8, " *Basi, vifisheni viungo vyenu vilivyo katika nchi, uasherati, uchafu, tama mbaya, mawazo mabaya, na kutamani, ndiyo ibada ya sanamu; kwa ajili ya mambo hayo huja ghadhabu ya Mungu. Katika hayo ninyi nanyi mlitembea zamani, mlipoishi katika hayo. Lakini sasa yawekeni mbali haya yote, hasira na ghadhabu, na uovu, na matukano, na matusi vinywani mwenu.*"

- Hali isiyo swari (tamaa)
- Mawazo mabaya (kutamani kitu ambacho umezuiwa).
- Kutamani (tama ya kuwa navyo vingi) ambayo ni ibada ya sanamu.
- Uchafu (kutaka kujeruhi).
- Matukano (uropokaji, maneno ya kujeruhi).
- Lugha chafu (kauli mbaya).

"*Kuvaa silaha za nuru*"

Ngao ya imani na upendo, tumaini la wokovu kama chapeo. 1 Thes. 5: 8, "*Lakini sisi tulio wa mchana, tuwe na kiasi, hali tukijivika kifuani imani na upendo, na chapeo yetu iwe tumaini la wokovu.*"

Silaha hiyo ya Mungu inajumlisha ukweli, haki, injili, imani, tumaini la wokovu, Neno la Mungu. Efe. 6: 10-17, "*Hatimaye mzidi kuwa hodari katika Bwana na katika uweza wa nguvu zake. Vaeni silaha zote za Mungu mpate kuweza kuzipinga hila za shetani. Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu war oho. Kwa sababu hiyo twaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kushindana siku ya uovu, na mkiisha kuyatimiza yote kusimama. Basi*

simameni hali mmejifunga kweli viunoni na kuvaa dirii ya haki kifuani, na kufungiwa miguu u tayari tupatao kwa Injili ya amani; zaidi ya yote mkiitwaa ngao ya imani, ambayo kwa hiyo mtaweza kuizima mishale yote yenye moto ya yule mwovu. Tena ipokeeni chapeo ya wokovu na upanga wa Roho ambao ni neno la Mungu."

"*Mjiweke ndani ya Bwana Yesu Kristo*"

Kwanza, katika ubatizo. Kwa sababu katika ubatizo "tunamvaa" Kristo. Gal. 3:27, "*Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo.*"

Tunafufuliwa "na" Kristo, "tunawekwa hai pamoja naye". Kol. 2:11-13, "*Katika yeye mmetahiriwa kwa tohara isiyofanyika kwa mikono kwa kuuvua mwili wa nyama, kwa tohara ya Kristo. Mkazikwa pamoja naye katika ubatizo, na katika huo mkafufuliwa pamoja naye; kwa kuziamini nguvu za Mungu aliyemfufua katika wafu. Na ninyi mlipokuwa mmekufa kwa sababu ya makosa yenu na kutokutahiriwa kwa mwili wenu aliwafanya hai pamoja naye, akiisha kutusamehe makosa yetu.*"

Hivyo, katika kuendeleza tabia inayofanana na Kristo.

Kuvaa utu mpya. Kol. 3:10-14, "*Mkivaa utu mpya unaofanywa upya upate ufahamu sawasawa na mfano wake yeye aliyeuumba. Hapo hapana Myunani wala Myahudi, kutahiriwa wala kutokutahiriwa, mgeni wala mshenzi, mtumwa wala mwungwana, bali Kristo ni yote katika yote. Basi kwa kuwa mmekuwa wateule wa Mungu, watakatifu wapendwao, jivikeni moyo wa rehema, utu wema, unyenyekevu, upole, uvumilivu, mkichukuliana na kusameheana, mtu akiwa na sababu ya kumlaumu mwenzake; kama Bwana alivyowasamehe ninyi, vivyo na ninyi. Zaidi ya hayo yote jivikeni upendo, ndio kifungo cha ukamilifu.*"

Mkiwa mmefanywa upya katika nia zenu, utu mpya katika kweli, haki na utakatifu. Efe. 4:20-24, "*Bali ninyi sivyo mlivyojifunza Kristo, ikiwa mlimsikia mkafundishwa katika yeye, kama kweli ilivyo katika Yesu, mvue kwa habari ya mwenendo wa kwanza utu wa zamani unaoharibika kwa kuzifuata tama zenye kudanganya; na mfanywe wapya katika roho ya nia zenu; mkavae utu mpya, ulioumbwa kwa namna ya Mungu katika haki na utakatifu wa kweli.*"

Kukua katika neema na ujuzi wa Yesu Kristo.

- 2 Pet. 1:5-8, "*Naam, na kwa sababu iyo hiyo mkijitahidi sana kwa upande wenu, katika imani yenu tieni na wema, na katika wema wenu maarifa, na katika maarifa yenu kiasi, na katika kiasi chenu*

saburi, na katika saburi yenu, utauwa, na katika utauwa wenu upendano wa ndugu, na katika upendano wa ndugu, upendo. Maana mambo hayo yakiwa kwenu na kujaa tele, yawafanya ninyi kuwa si wavivu, wala si watu wasio na matunda."

- 2 Pet. 3:18, "*Lakini kueni katika neema, na katika kumjua Bwana wetu na Mwokozi Yesu Kristo. Utukufu una yeye sasa na hata milele.*"

"*Tusijitoe kwa ajili ya mwili*"

Kitu ambacho lazima tukifanye!

Kama tunataka kuishi kiroho. Rum. 8:12-13, "*Basi kama ni hivyo ndugu tu wadeni, si wa mwili tuishi kwa kufuata mambo ya mwili, kwa maana kama tukiishi kwa kufuata mambo ya mwili, mwataka kufa; bali kama mkiyafisha matendo ya mwili kwa Roho, mtaishi.*"

Kama tunatamani upendo wa Baba. 1 Yoh. 2:15-17, "*Msiipende dunia wala mambo yalimo katika dunia, mtu akiipenda dunia kumpenda Baba hakumo ndani yake. Maana kila kilichomo duniani, yaani, tamaa ya mwili, na tamaa ya macho, na kiburi cha uzima, havitokani na Baba, bali vyatokana na dunia. Na dunia inapita pamoja na tama zake, bali yeye afanyaye mapenzi ya Mungu adumu hata milele.*"

Kitu ambacho tunaweza kufanya!

Kwa msaada wa Roho.

- Rum. 8:13, "*kwa maana kama tukiishi kwa kuufuata mambo ya mwili, mwataka kufa; bali kama mkiyafisha matendo ya mwili kwa Roho, mtaishi.*"
- Efe. 3:16, "*Awajalieni kwa kadiri ya utajiri wa utukufu wake, kufanywa imara kwa nguvu, kwa kazi ya Roho yake katika utu wa ndani.*"
- Efe. 3:20, "*Basi atukuzwe yeye awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo, au tuyawazayo kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu.*"
- Gal. 5:16-17, "*Basi nasema enendeni kwa Roho wala hamtazitimiza kamwe tama za mwili. Kwa sababu mwili hutamani ukishindana na Roho, na Roho kushindana na mwili; kwa maana hizi zimepingana, hata hamwezi kufanya mnayotaka.*"

Kwa msaada ambao Mungu anatoa. 1 Kor. 10:13, "*Jaribu halikuwapata ninyi, isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu; ila Mungu ni*

mwaminifu ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo; lakini pamoja na lile jaribu atafanya na malango ya kutokea, ili mweze kustahimili."

Kwa msaada wa maombi ya kukesha.

- Mt. 26:41, "*Kesheni mwombe, msije mkaingia majaribuni; roho I radhi lakini mwili ni dhaifu.*"
- 1 Pet. 4:7, "*Lakini mwisho wa mambo yote umekaribia; basi iweni na akili, mkeshe katika sala.*"
- 1 Pet. 5:8, "*Mwe na kiasi na kukesha; kwa kuwa mshitaki wenu ibilisi kama samba angurumaye, huzunguka zunguka akitafuta mtu ammeze.*"

Katika mtazamo huu tuko makini kiasi gain?

Je tunahepuka mazingira ambayo yanaweza kuujaribu mwili? Je tunaondokana na matendo ambayo yanaibua tama ya mwili?

Hitimisho

Ndugu, je tunalala? Utofauti katika mambo ya roho, kutokuwa makini na mambo ya milele? Wazito katika huduma yetu kwa Bwana, na kutojali uimara wetu wa kiroho.

Kama ndivyo, basi "Ni Wakati Wa Kuamka!"

Wakati wa kubadilika na kukua utatoweka haraka! Siku ya milele itawadia na hatutakuwa tayari!

Tuwe wana wa nuru, na si wa giza. Mvae Bwana Yesu. Vaa silaha za nuru. Tembea sawasawa.

Usijitoe kwa ajili ya mwili ili kutimiza tama za kimwili, na tunaweza kuangalia mbele ili kuweza kuupata wokovu kupitia Yesu Kristo! 1 Thes. 5:1-11, "*Lakini ndugu kwa habari ya nyakati na majira, hamna haja niwaandikie. Maana ninyi wenyewe mnajua yakini ya kuwa siku ya Bwana yaja kama vile mwivi ajavyo usiku, wakati wasemapo kuna amani na salama, ndipo uharibifu uwajiapo, kwa ghafla kama vile utungu umjiavyo mwenye mamba, wala hakika hawataokolewa. Bali ninyi ndugu hammo gizani, hata siku ile iwapate kama mwivi. Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa wana wa nuru, na wana wa mchana; sisi si wa usiku wala wa giza. Basi tusilale usingizi kama na wengine, bali tukeshe, na kuwa na kiasi. Maana walalao usingizi hulala usiku, pia na walewao ulewa usiku. Lakini sisi tulio wa mchana, tuwe na kiasi, hali tukijivika kifuani imani na upendo, na chapeo yetu iwe tumaini la wokovu. Kwa maana Mungu hakutuweka kwa hasira yake, bali tupate wokovu, kwa Bwana wetu Yesu Kristo; ambaye alikufa kwa ajili yetu, ili tuishi pamoja naye, kwamba*

twakesha au kwamba twalala. Basi farijianeni na kujengana kila mtu na mwenzake, vile vile kama mnavyofanya."

Tunafanyaje hili liwezekane? Kwa kuwa Mkristo. Zifuatazo ni hatua muhimu kufanya hili liwezekane:

- **Imani.** Ebr. 11:6, "*Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao.*" Nilipokuwa katika shule ya upili (nilikuwa na miaka 17), kijana mmoja miaka sawa na yangu akaniambia alikuwa haamini kwamba Mungu yupo. Kwa vile nilikuwa nimebatizwa, nilichukua nafasi ya kuongea naye kuhusu maandiko. Akanijibu kuwa anaweza kuona kwamba kuishi maisha ya Ukristo ni nzuri, lakini hakuwa na uhakika kwamba Mungu yupo. Lakini ili awe sehemu nzuri, labda aende kanisani, na atakapo kufa na kusimama mbele za Mungu (kama kuna Mungu) siku ya hukumu (kama kuna hukumu), labda kama Mungu akiona kwamba anakwenda kanisani na kuishi maisha mema Mungu atamruhusu kuingia mbinguni (kama kuna mbingu), na sio motoni (kama kuna moto). Nikamwambia, "swala hili halifanyi kazi kwa njia hiyo. Unapaswa kumwamini kwa moyo wako wote bila hivyo huwezi kumuamini."

- **Toba.** Mdo. 2:38, "*Petro akawaambia tubuni, mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*" Mdo. 11:18, "*… basi Mungu amewajalia hata mataifa nao toba liletalo uzima.*" Kama ulikuwa unalala, ukasikia sauti katika chumba nyingine, n akufikiria mwenyewe, "mwizi ameingia ndani!" Na unachukua simu yako, kwa utaratibu unavyoweza, unawaita polisi, ukiwaambia kwamba kuna mwizi ndani mwako, na unawapa anuani yako. Muda mfupi unawasikia wamefika, na kumkamata mwizi. Anapiga kelele. "Samahani; samahani!" msamaha ni wa nini? Anaomba msamaha kwa sababu ameshikwa; na sio kwamba ameiba. Katika toba ya kweli mwizi angeomba msamaha kwamba hataiba tena na kwamba anataka kubadili maisha yake ili kwamba asije akaiba tena. Hiyo ndiyo toba ya kweli. Hicho ndiyo tunatakiwa kukifanya kabla hatujafanyika Wakristo.

- **Kiri.** Rum. 10:9-10, "*Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.*" Tuna kiri nini? Kwamba tunaamini kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu.

Kumbuka kwamba katika andiko hilo hapo juu kwamba imani (kuamini), toba, na kukiri ni "**KATIKA"** haki, uzima au wokovu. "Katika" inamanisha kuelekea kitu fulani; siyo kwamba mtu tayari ameshapata.

- **Ubatizo.** Ni katika ubatizo ndipo haki, uzima, na wokovu vinapatikana. Yesu, mwenyewe, alibatizwa kuitimiza haki yote. "*lakini Yohana alitaka kumzuia, akisema mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia kubali hivi sasa; kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akamkubali. Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini, na tazama mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua akija juu yake; na tazama sauti kutoka mbinguni ikisema, Huyu ni Mwanangu mpendwa wangu, ninayependezwa naye.*" (Mt. 3:14-17). Yesu alibatizwa kwa sababu Mungu alisema ni kitu sahihi kukifanya. Unaona jinsi Mungu alivyopendezwa Yesu alipobatizwa? Yesu pia akasema "*kwa kuwa ndivyo* ***itupasavyo*** *kuitimiza haki yote.*" Tunabatizwa kwa sababu inatimiza haki yake, siyo kwa sababu ni haki yetu.

  Kwa kweli, kama hatuja batizwa, bado tungali katika dhambi zetu. "*Petro akawaambia tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*" (Mdo. 2:38). Petro, umesema ni nini kusudi la ubatizo? "*kwa ajili ya ondoleo la dhambi*". Kwa nini mtu yeyote anataka kuondoa hatua inayoondoa dhambi zetu?

  Yesu aliagiza kwamba kuweza kuufikia wokovu lazima tubatizwe. "*Akawaambia enendeni ulimwenguni kote mkahubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye* ***na*** *kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa.*" (Mk. 16:15-16).

  Anania alimwambia Sauli (kabla hajaitwa Paulo) kitu kama hiki, "*Basi sasa unakaawilia nini? Simama ubatizwe, ukaoshe dhambi zako, ukiliitia jina lake.*" (Mdo. 22:16). Ubatizo ni hitaji kutoka kwa Mungu.

  Ubatizo unaitwa maziko. "*Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu, kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaunganika kwa mfano wa kufufuka kwake; mkijua neno hili ya kuwa, utu wetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena.*" (Rum. 6:3-6).

Ubatizo ni ramani ya Mungu ya kutumia damu ya Kristo katika maisha yetu kwa ubatizo. Tunakuwa huru kutoka katika dhambi zetu za zamani pale tu tunapo batizwa.

Hii haimanishi, “kunyunyiza. Andiko hapo juu inaseama ubatizo ni maziko. Hatupeleki mwili makaburini na kuuwekea udongo kidogo juu yake; bali tunauzika.

Kama hujafanyika Mkristo, kwa nini usizingatie leo?